

Maswali na Majibu

1. Manabii walikuwa wakijua namna gani mambo yatakayokuweco baadaye?
Mungu aliwaonyesha. Mungu anajua kila kitu na yeye ana amri ya yote.
2. Nani ndiye mtu wa kipekee mwenye manabii walizungumzia? *Yesu*
3. Masiya ina maana gani?
Mtu anayepakwa mafuta awe mfalme.
4. Manabii walisema nini juu ya Mariamu? *Atakuwa bikira.*
5. Hii ilitimizwa namna gani?
Yesu alizaliwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.
6. Manabii walisema Yesu atazaliwa wapi? *Bethlehemu*
7. Manabii walisema Yesu atafanya nini?
Ponya wagonjwa, vipofu, viwete na kufufua wafu
8. Manabii wanatwambia nini juu ya kifo cha Yesu?
Atasulibiwa, atadhihakiwa, watapiga kura kwa mavasi yake, atakufa na wezi, azikwe na mtu tajiri na afufuliwe.
9. Manabii walisema Yesu atakuwa Mfalme. Atakuwa lini?
Atakaporudi hapa duniani.
10. Ufalme wa Mungu utakuwa namna gani?
Utakuwa na Nchi yenye rutuba. Hakutakuwa na maumivu wala matezo. Hakutakuwa na vita. Kutakuwa na amani na haki. Wote watampenda Mungu na kumtii. Kutakuwa na furaha na shangwe.

Mistari ya kukariri

Isaya 7:14 Zaburi 22.1 Isaya 35:5 – 6 Isaya 11:9

Mazungumzo

Wale watakaokubaliwa kwa Ufalme watasaidia Yesu kufanya ulimwengu kuwa mahali pa ajabu. Zungumza vile ulimwengu utabadilika. Wewe mwenyewe utasaidia Yesu kufanya nini?

Kuandika

Soma Mathayo 1:18 – 2:23 **AU** Zaburi 22. Andika vile Yesu alitimiza unabii wa hizi mistari.

Masomo ya watoto wakubwa wa CBM



Somo la 30 Unabii kuhusu Yesu

SOMA Isaya 35 na somo lenyewe

SOMO

Tumejifunza kwa masomo yaliyopita juu ya ahadi za Mungu kwa Adamu, Ibrahimu na Daudi. Mungu aliahidi watu wake kwamba siku moja mtu muhimu atazaliwa. Huyu mtu atawapa watu matumaini ya maisha na siku moja atatawala mataifa yote kutoka Yerusalemu.

Wayahudi walitazamia sana wakati huyu mtu atakuja. Walimwita Masiya. Neno 'Masiya' maana yake ni 'mtu aliyepakwa mafuta'. Katika Israeli, mtu alipakwa mafuta kuwa mfalme. Samweli alipaka Sauli na Daudi mafuta kuwa wafalme. Masiya mwenye ameahidiwa atakuwa mfalme wa Wayahudi na ulimwengu mzima. Huyu Masiya si mwingine ila ni Yesu. Manabii wanatwambia mengi sana kuhusu huyu Masiya na Ufalme wenye atasimamisha.

Manabii walisema kwamba Masiya atazaliwa kwa njia ya kipekee. Kuna baadhi ya watu wengine kwa Biblia waliozaliwa kwa njia isio ya kawaida – Isaka alizaliwa na Sara wakati alikuwa mzee. Samweli alizaliwa na Hana baada ya kuwa tasa. Lakini kuzaliwa kwa Masiya ni tofauti kabisa.

📖 Soma Isaya 7:14 – 16. Mungu aliambia huyu nabii Isaya kwamba Masiya atazaliwa na bikira. Hatakuwa na baba wa kidunia. Mimba yake haitapatikana kama kawaida. 📖 Luka 1:26 – 32. Mariamu mama wa Yesu alikuwa bikira. Mariamu alipata mimba ya Yesu kupitia kwa nguvu za Roho Mtakatifu. Mungu ndiye Baba wa Yesu.

Manabii walisema hata mahali penye Yesu atazaliwa. 📖 Mika 5:2 anatwambia kwamba atazaliwa Bethlehemu. 📖 Mathayo 2:1 – 6. Makuhani wakuu walijua huu unabii walipoambia Herode kwamba Yesu atazaliwa Bethlehemu.



Masiya atafanya nini atakapokuja? 📖 Soma Isaya 61:1 – 2. Atafundisha watu habari njema juu ya wokovu wa Mungu. Atasaidia maskini, atawapa watu tumaini la uzima kwa Ufalme wa Mungu hapa duniani kwa sababu watakuwa huru kutoka kwa dhambi na mateso. 📖 Soma Luka 4:16 – 21. Kuna siku Yesu alikuwa kwa Sinagogi na aliulizwa kusoma. Alisoma mistari kutoka kwa Isaya. Halafu akaambia watu, “Leo hii haya maneno yametimia.”

📖 Soma Isaya 29:18 na 35:5 – 6. Hapa inatwambia vipofu wataona, viziwi watasikia na viwete watatembea. Yesu aliponya watu wengi sana - kipofu Bartimayo, mlema kwa birika ya Siloamu na wengine wengi, wengi sana. Yohana alipokuwa gerezani alituma watu waulize kama yeye ndiye Masiya. Yesu alituma wamwambie Yohana kazi yenye alikuwa akifanya – anafanya vipofu wanaona, viziwi wanasikia, viwete wanatembea, wafu wanafufuliwa na anahubiria maskini.

Unabii unatuelezea kiundani sana vile Masiya atakufa. Zaburi 22 inazungumzia kifo cha Yesu. 📖 Soma Zaburi 22:1 – 18 tena Mathayo 27:41 – 44 kuona vile unabii ulitimizwa.

Yesu alipokuwa akikata roho, akifa alipaza sauti, “ Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?” Alikuwa ananakili Zaburi 22 mstari wa 1. Mistari ya 7 na 8 inatwambia kwamba Yesu aliteswa na kudhulumiwa. Watu watasema, “Aliamini Mungu, wacha Mungu amwokoe.” Mstari wa 16 unasema kwamba mikono yake na miguu itatobolewa. Tunajua kwamba mikono na miguu ya Yesu ilipigiliwa msabani kwa misumari. Hii inatwambia kwamba Yesu atakufa kwa kusulibiwa, ingawaje kusulibiwa hakukuwepo wakati Zaburi iliandikwa. Mstari wa 18 unatwambia kwamba nguo za Yesu zitagawanywa kwa kupiga kura. Askari walifanya hivyo nguo za Yesu. Unabii huu wote ulitimizwa wakati Yesu alipokuwa akifa.

📖 Soma Isaya 53, nayo pia inatwambia juu ya kifo cha Yesu. Mstari wa 7 unasema, kwamba vile aliumizwa na kupigwa, hakufunua kinywa chake. Wakati makuhani na wakuu waliposhitaki Yesu, hakusema kitu. Mstari wa 9 unasema kwamba atapewa kaburi pamoja na waovu tena pamoja na matajiri wakati wa kifo chake. Yesu alisulibiwa na wezi wawili. Angetupwa penye watu wanaosulibiwa walikuwa wakitupwa kule Gehena iliyoko Yerusalemu kwenye mlima wa takataka nyingi. Lakini Yusufu wa Arimathaya, mtu tajiri, aliomba kupewa mwili wa Yesu na akauzika kwa kaburi lake. Kwa hivyo unabii wa watu waovu na matajiri ulikuwa umetimizwa.


Mstari wa 11 unasema kwamba baada ya kifo chake ataona mwangaza wa uzima na atatosheka. Yesu alifufuliwa kutoka kwa wafu na alifurahi akijua kwamba kwa kifo chake watu wanaopenda Mungu na kumtii watapata uzima. Kifo cha Yesu kilituchukulia dhambi zetu tena ndiye mpatanishi (ako katikati ya Mungu na watu) wa wenye dhambi.

Kuna unabii wenye haukutimizwa wakati alikuwa hai tena kwa kifo chake. Kutokana na ahadi kwa Daudi kwamba Masiya (Yesu) atakuwa Mfalme wa dunia nzima kutokea Yerusalemu. Bado Yesu hajakuwa Mfalme. Unabii huu ungali wa baadaye. Yesu atakuwa Mfalme, wakati atarudi hapa duniani kusimamisha Ufalme wa Mungu.

Kuna unabii mwingi sana unaotwambia juu ya Yesu kusimamisha Ufalme wa Mungu hapa duniani. 📖 Isaya 35. Mlango huu unazungumzia Ufalme.

Mstari wa 1, 2 na 7 zinatwambia kwamba Yesu atatawala ulimwengu utakaokuwa na chakula kingi. Dunia itakuwa ya rutuba sana. Mavuno yatakua mengi. Kutakuwa na mvua ya kutosha. Nchi itakuwa na rutuba nyingi mpaka milimani kutakua nafaka, hata jangwani kutatoa maua.

Mstari wa 5 na 6 zimetabiri kwamba hakutakuwa na maumivu wala kifo. Watu hawatakuwa wagonjwa. Vipofu wataona, viziwi watasikia na viwete watatembea. Uponyaji wa Yesu utatumiwa kuponya watu wote duniani.



📖 Soma Mika 4:2 – 4. Watu wote watajifunza kumpenda Mungu na kutii amri zake. Hakutakuwa na vita kwa sababu watu watapenda Mungu na wataishi kwa amani na majirani wao. Watu hawatajifunza kupigana tena. Hakutakuwa na haja ya silaha za vita na watavitumia kama vifaa vya ukulima. Hata wanyama wa mwitumi watafugwa na hawataumiza watu. Watoto watacheza nao. (Isaya 11:6 – 9 na Isaya 35:9)

Watu katika Ufalme wa Mungu watakuwa na furaha na shangwe kuu. Hakutakuwa na huzuni hata kidogo. Yesu atakuwa Mfalme mzuri. Atatawala kutoka Yerusalemu mpaka dunia nzima. Hebu sote tuombe ili akuje mapema.

